

*Ndaki ahimiza tafiti zenye tija kwa wafugaji

Na Anastazia Anyimike,
Dodoma

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kushiriki kikamilifu katika tafiti zitakazoleta tija kwa wafugaji wakati serikali ikielekea kuwa na sera mpya ya mifugo. Ndaki, alibainisha hayo

jijini hapa wakati wa kuzindua Bodi ya Taliri na kubainisha kuwa ni vigumu kuwa na sera bila kuwa na tafiti.

Alisema taasisi hiyo inapaswa kufanya tafiti hizo kwa kuzingatia maelekezo, ubora na mahitaji ya wafugaji kwa kuwa mahitaji ni mengi na changamoto ni nyingi zinazohitaji utatuzi.

Alisema masuala ya mabadiliko ya tabianchi, masoko ya bidhaa za mifugo, uzalishaji na biashara ya

mifugo ni baadhi ya masuala muhimu ambayo yanatakiwa kujumuishwa kwenye sera ya mifugo.

"Sera ni lazima ituelezee namna ya kuendesha sekta ya mifugo tukizingatia wingi wa shughuli za binadamu, mazingira ya sasa, masoko ya bidhaa za mifugo na biashara ya mifugo," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taliri, Profesa Sebastian Chenyambuga alisema bodi itahakikisha inasimamia

masuala ya utafiti kadri inavyotakiwa kwa kutoa matokeo ya namna ya kuendesha sekta ya mifugo na kutatua changamoto zilizopo.

"Nikuahidi bodi itasimamia kwa karibu Taliri kufanya tafiti za masuala yanayohusu sekta ya mifugo ikiwamo yale yanayoibuka na mengine kusababisha taharuki kwa wananchi," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda aliwataka wajumbe

wa bodi kuwa na mpango wa upatikanaji wa fedha ili kupata rasilimali fedha kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali.

Alisema bodi ni lazima ije na mpango wa mabadiliko ya taasisi hiyo ambao unalingana na mahitaji ya sasa wenye kushirikisha sekta binafsi wakiwamo wachakataji na wazalishaji wa viwandani.

Bodi ya Taliri iliyozinduliwa rasmi juzi itakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu.